Evangelical Lutheran Church in Tanzania-KARAGWE DIOCESE

KARAGWE SECONDARY SCHOOL

P.O. Box 87, Karagwe, TANZANIA, Phone:+255 784 301 342
Fax: +255 028 2223262.E-mail karaseco@mail.com; web: www.karaseco.co.tz

Ref. SSK/ ***Tarehe:……***

Bwana/Bibi:…….
Mzazi/Mlezi wa:……..
…….
…….

Yah: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KARAGWE (KARASECO)

1. (a) Ninafurahi kukujulisha kuwa mwanao:……... amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Karagwe kidato cha **Tano 2016** Shule itafunguliwa tarehe: **06. 10.2016** Mtoto wako anapaswa kufika shuleni tarehe hiyo kabla ya saa **9.00** alasiri. Akichelewa zaidi **wiki mbili** nafasi yake atapewa mtu mwingine.

   (b) Inahusu Kidato cha Tano: Amechaguliwa/amekubaliwa kuchukua masomo yafuatayo (subject combination):

   (i). HGL ☐ (ii).HGK ☐ (iii). HKL ☐ (iv).HGE ☐ (v). EGM ☐
   (vi). CBG ☐ PCB ☐ PCM ☐ PGM ☐

2. Shule ya Sekondari Karagwe iko mahali panapoitwa **Kamagombe** katika Kijiji cha **Kishojo,** kilometa **12** kutoka **Kayanga,** mji mkuu wa Wilaya, na **kilometa moja** kutoka barabara itokayo Kayanga kwenda Bukoba Mjini.

3. Hii ni shule ya bweni na ya mchanganyiko (Boarding and Co-educational School). Wanafunzi wote hulala shuleni.

4. **(a) KARO: Tazama kiambatanisho.**
   (b) MAHITAJI MENGINE/MUHIMU:
   (i) Godoro lenye upana wa futi 2½ na unene wa inchi 4 au 6. Aina ya DODOMA au SUPER BANKO (JIPYA).

   (ii) Oxford Student's Dictionary of English/Oxford Advanced Learner's Dictionary.
   .

   (iii) Rimu moja ya karatasi nyeupe (photocopy) A_4

5. **SARE:**
   (a) (i) **Wasichana** – Wanatakiwa wawe na sketi mbili nyeusi zenye malinda, ndefu kuanzia kitovuni hadi chini ya mogoti, zisizoang'avu (not transparent) na mashati mawili meupe mikono mifupi, viatu vya ngozi rangi nyeusi tu na stocking nyeupe.
   Mavazi nje ya darasa – sketi mbili rangi ya damu ya mzee zenye malinda, ndefu za heshima.

(ii) **Wavulana** – Suruali mbili nyeusi, mashati mawili meupe mikono mifupi yasiyoang'avu (not transparent), viatu vya ngozi rangi nyeusi na soksi nyeusi.

Mavazi nje ya darasa – suruali mbili rangi ya damu ya mzee.

(b) (i) **Malazi/Matandiko**: Shuka rangi ya pinki wasichana 2 – Bluu wavulana 2, blanketi 1, mto 1, foronya 2.

Vifaa vingine: Kotama au fyekeo 1, ndoo 1 ya plastiki ya lita 20, jembe na mpini wake 1, kijiko, mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set), rula, kalamu za wino, madaftari ya kutosha, sabuni za kuogea, kufuli 2 (moja kufungia dawati lake darasani na ya pili ya kufungia kabati lake bwenini), mswaki na dawa ya meno, mafuta ya ngozi/nywele, taulo 1, mfuko wa kubebea vifaa vya masomo., Chandarua, Nguo za kulala (Night Dress/Pyjamas), Sanduku imara la kuhifadhia mali zake na Toilet papers (karatasi za chooni). pkt 5

Kwa wasichana waje na track suit rangi ya kijivu kwa ajili ya kuvaa wakati wa maandalizi ya usiku..

(ii) Mavazi/Vazi la michezo:

Kila mwanafunzi alete viatu/raba za michezo.

.

6. **M U H I M U**: a) Kofia, mikufu, hereni, pete, viatu vyenye visigino virefu na mapambo mengine ni marufuku kuvaliwa shuleni. Makoti, jaketi si sehemu ya sare, hivyo havitaruhusiwa shuleni. Wenye matatizo ya kiafya wataruhusiwa kuvaa sweta wakati wa baridi. Ni lazima mwanafunzi avae sare ya shule wakati wa:
   (i) Masomo darasani.
   (ii) Kutoka nje ya shule.
   (iii) Mihadhara ya shule.

   Zingatia:
   - Nywele lazima ziwe fupi. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara au panki.
   -Kucha zikatwe na zisipakwe rangi/ina.
   -Ufugaji wa ndevu na uvaaji wa mapambo hauruhusiwi.
   -Kuvaa mlegezo wa sketi na suruali au shati za kubana **HAVIRUHUSIW**I.
   - Sketi fupi haziruhusiwi.

7. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vya dini, sala na ibada kulingana na utaratibu wa shule. .

8. (i) Mwanafunzi atakapofika shuleni aonane na mwalimu wa zamu/bweni au Mwandamizi Malezi. Atakabidhiwa kitanda, dawati na pia vyombo vya chakula na atawajibika kuvitunza.

   Shule yetu ni ya mchepuo wa kilimo, kwa hiyo sehemu kubwa ya mafunzo ya nje itahusika na **kilimo,** ufugaji na kazi nyingine za kujenga Taifa. Kila mwanafunzi atapaswa kuzithamini kazi hizi kama sehemu ya masomo yake.

   (ii) L i k i z o: Kutakuwa na likizo ndefu ambazo utajulishwa katika ripoti ya kila muhula ya mtoto wako. Pia ipo likizo fupi ya wiki moja katikati ya kila muhula. Likizo hii fupi si haki ya mwanafunzi kwenda nyumbani. Shule itakuwa na uamuzi wa kuwabakiza vijana wa vidato fulani fulani ili kupewa mafunzo ya ziada au wahudumie miradi ya shule wakati wa likizo hizo fupi.

   (iv) N i d h a m u: Wazazi wa mtoto hawana budi kuelewa kuwa nidhamu ni kitu muhimu shuleni. Mtoto akikosa nidhamu mfano: **utoro, uzembe, uzinzi wizi, kiburi na kutopenda kushirikiana na wenzake**, shule haitasita kumrudisha nyumbani.

   (iv) **V i f o**: Mwanafunzi ataruhusiwa tu kwenda kwenye kilio iwapo atakuwa amefiwa na mzazi/mlezi anayetambuliwa shuleni. Ruhusa hii haitazidi siku **7**

(saba). Vilio vingine vya ndugu/jamaa au rafiki, mwanafunzi ataomboleza hapa hapa shuleni. Lengo letu ni kumsaidia asipoteze masomo.

(v) **Wito Shuleni**: Mzazi unaombwa kuwa tayari kuitikia wito wa shule au kuhudhuria mikutano ya wazazi au kushirikiana na uongozi wa shule kutatua matatizo ya mtoto wako.

(vi) **F e d h a:** Mzazi huna budi kumnunulia mtoto wako vifaa vinavyohitajiwa shuleni kuliko kumpa fedha nyingi ambazo zinaweza kumuingiza vishawishini.

(vii) **C h a k u l a**: Hutolewa na shule hivyo vyakula vingine kutoka nje ya shule haviruhusiwi.

9. Mambo ya kufanya kabla ya mwanafunzi kufika shuleni:
   (i) Aje na cheti cha kuzaliwa.
   (ii) Fomu Na. **SSF.2** ya usajili wa mwanafunzi ijazwe na wahusika wote na kuwekwa picha.
   (iii) Fomu Na**. SSF.3** ya kukubali kujiunga na shule hii ijazwe na kusainiwa.
   (iv) Fomu ya kupimwa Na. **SSF.4** iliyoambatanishwa ijazwe na Daktari Mkuu wa Hospitali inayotambuliwa na Serikali.
   (v) Mwanafunzi anayekuja kujiunga na kidato cha 5 aje na matokeo yake ya kidato cha nne (result slip). Mwanafunzi hatapokelewa kama hana matokeo halisi.
   (vi) Kabidhi fomu hizi kwa Mwalimu Mwandamizi Malezi mara ufikapo shuleni. Hatapokelewa shuleni kama hukuzikamlisha.

10. **<u>MUHIMU KUZINGATIA</u>:** MWANAFUNZI AKIWA SHULENI ATAFUATA KANUNI NA SHERIA ZA SHULE.
    Sheria, kanuni na taratibu za shule, mtoto wako atazikuta shuleni. Atatakiwa kuzisoma kwa makini: akizikubali ataweka saini yake na kupokelewa shuleni; akizikataa atarudishwa nyumbani.

ELIMU NI UKOMBOZI.

KARIBU SANA "KARASECO"

<u>MKUU WA SHULE</u>

USAJILI WA MWANAFUNZI **SSF.2**

TAREHE:……

PICHA
(PASSPORT SIZE)

Jina kamili la mwanafunzi (kama kwenye mtihani)……
Shule utokayo…….Namba ya Mtihani:……..
Mwaka uliofanya mtihani:……..

Jinsi: Msichana/Mvulana (kata isiyohusika)
Tarehe ya kuzaliwa……..Kijiji/Mji……..Wilaya……
Dini……Dhehebu……
Kidato unachokuja kuingia hapa shuleni:…….
Jina kamili la Baba:……..
Jina kamili la Mama…….
Jina kamili la Mlezi kama huna wazazi……
Uhusiano wa mlezi…….
Kazi ya baba/mama/mlezi……..
Namba ya simu:……E-mail…….Fax……...

Jamaa katika familia:

b) Idadi ya Wavulana ☐
c) Idadi ya Wasichana ☐
d) Wewe ni mzaliwa wa ngapi katika familia. ☐

Unaishi na nani:

(i). Wazazi wote wawili (ii). Mama tu. (iii). Baba tu. (iv). Mlezi (weka tick ( ) kwenye sehemu inayohusika).

Dini ya Baba……

Dini ya Mama…….

Dini ya Mlezi……

Saini ya Mwanafunzi……Tarehe……

Saini ya Mzazi/Mlezi……..Tarehe……

SSF. 3

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KARAGWE

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi……ninakubali/sikubali kujiunga na Shule ya Sekondari Karagwe katika Kidato cha……/Combination ya…… (inahusu kidato cha 5 tu). Kila mara nitafika shuleni bila kuchelewa na ninaahidi kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zote za shule.

Saini ya Mwanafunzi…….Tarehe……

B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi……ambaye ni mzazi/mlezi wamtotoninakubali/sikubali mtoto wangu ajiunge na Shule ya Sekondari Karagwe kuanzia tarehe……. Ninaahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama shule ilivyoagiza.

Nitakuwa tayari kuhudhuria mikutano ya wazazi au kuitikia wito wa shule na kushirikiana na uongozi wa shule kutatua matatizo ya mtoto wangu pindi yatokeapo. Nitakubaliana na hatua za kinidhamu atakazochukuliwa mwanangu pale atakapobainika kukiuka kanuni, taratibu au sheria za shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi…….Tarehe:……

Malipo yafanyike kupitia benki, kwenye akaunti zifuatazo:

1. Shule ya Sekondari Karagwe Akaunti Na. 31903500022 – NMB, Tawi la Kayanga .
2. Shule ya Sekondari Karagwe Akaunti Na. 01J1090513900 – CRDB, Tawi la Karagwe .

N.B: Pay in slip hati ya malipo halisi iletwe shuleni.

Ahsante kwa ushirikiano katika jambo hili muhimu.

N.B: Mwanafunzi hatapokelewa asipokamilisha malipo ya awamu husika.

MKUU WA SHULE

Evangelical Lutheran Church in Tanzania-KARAGWE DIOCESE
KARAGWE SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 87,Karagwe, TANZANIA, Phone:+255 0784 301 342
Fax: +255 028 2223262. E-mail karaseco@mail.comWeb:www.karaseco.co.tz

Ref. ***Date……***
SSF.4

FULL NAME:……..

PART A:
To the Medical Officer,
……
……
……

Please examine the above named student as to his/her physical & mental fitness/unfitness for admission as a full-time student. The examination should include the following categories: Eyesight, hearing, speech, limbs, venereal diseases, epilepsy, urine examination and stool examination.

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by The Medical Officer)

I have examined the above student and found him/her with the following impairment/disabilities:

(i) Eyesight……(ii) Limbs……
(iii) Hearing……. (iv) Venereal diseases……
(v) Epilepsy……...(vi) Speech……
(vii) Urine examination……(viii) Stool examination……
(ix) Additional information/other serious diseases……...
……
……
Treatment after examination (please state the nature of treatment)……..
……
……
I certify that the above-mentioned student has been examined and found fit/unfit to pursue further education.

Name:……Signature:……

Station……..Designation……..

Date……..Official Stamp……..

Evangelical Lutheran Church in Tanzania-KARAGWE DIOCESE
KARAGWE SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 87,Karagwe, TANZANIA, Phone:+255 784 301 342
*Fax: +255 028 2223262. E-mail karaseco@mail.com*Web:
www.karaseco.co.tz

UTARATIBU WA KULIPA KARO MWAKA 2017

KIDATO CHA KWANZA, 2017

I	JANUARY	580,000.00
II	APRIL	270,000.00
III	JULAI	400,000.00
IV	SEPTEMBA	250,000.00
	JUMLA	**1,500,000.00**

MUHIMU:

1. Karo ilipwe kila mwanzo wa awamu shule inapofunguliwa kama inavyoainishwa kwenye jedwali.

2. Malipo yote yafanyike kupitia Benki ya CRDB A/C.No. 01J90513900 AU NMB A/C No. 31903500022.

3. Aje na Ream moja ya Karatasi nyeupe (Photocopy A4) kwa kila mwanzo wa muhula.

4. Ada haitarudishwa endapo mwanafunzi atahama au kufukuzwa kwa makosa ya kinidhamu.

SOPHIA L. KANYAMWENGE
MKUU WA SHULE